**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BIMA TANZANIA (TIRA)

**Mei 6, 2025**

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

### PONGEZI KWA JESHI LA POLISI KWA KUBAINI UDANGANYIFU KATIKA BIMA

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) inatoa pongezi za dhati kwa Jeshi la Polisi Tanzania kwa ufanisi mkubwa na weledi katika kutekeleza majukumu yake ya kulinda usalama na kushughulikia uhalifu kwa mafanikio.

Hivi karibuni, Jeshi la Polisi limebaini na kufichua njama ya mtu mmoja aliyejulikana kwa jina la **David Zefania Sanga** anaedaiwa kutoa taarifa za uongo kwamba aliibiwa vifaa kutoka kwenye magari yake mawili, kwa lengo la kupata malipo ya madai ya uongo kutoka kwa kampuni za bima, vifaa ambavyo polisi walivikuta nyumbani kwake.

Tukio hili lililohusisha nia ya udanganyifu dhidi ya Sekta ya Bima, linadhihirisha kiwango kikubwa cha uchunguzi na ufuatiliaji makini unaofanywa na Jeshi la Polisi. Kwa umahiri na juhudi za askari wetu, mtu huyo amebainika na anashikiliwa na Jeshi la Polisi.

Kwa niaba ya Sekta ya Bima nchini natoa pongezi za dhati kwa Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri ya kulinda haki, kuimarisha uwajibikaji na kuhakikisha kuwa wahalifu wanabainishwa na kuwajibishwa ipasavyo. Ufanisi huu ni uthibitisho kuwa Tanzania ina vyombo vya dola vyenye uwezo wa hali ya juu na vinavyofanya kazi kwa uadilifu na kwa kuzingatia maslahi ya umma.

TIRA inaendelea kuwasisitiza wananchi wote kujiepusha na vitendo vya udanganyifu katika bima kwani kwa ushirikiano wa karibu na vyombo vya ulinzi na usalama TIRA inaendelea kuimarisha mifumo yake ya kuzuia na kubaini matendo ya udanganyifu na hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa atakaebainika kujihusisha au kushiriki kwa namna yeyote kwenye udanganyifu.

**Imetolewa na:**

**Dkt. Baghayo A. Saqware**

**Kamishna wa Bima**
**Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania(TIRA),**


**TIRA HEAD OFFICE**
LAPF HOUSE, 5th Floor, Makole Street,
P.O. Box 2987 DODOMA, Tanzania,
Tel: +255 26 2321180,
Fax: +255 26 2321180,
Website: www.tira.go.tz,
Email: coi@tira.go.tz

**Dar es salaam Sub-Office**
TIRA House Block 33
Plot No: 85/2115, Mtendeni Street,
P.O.BOX 9892, Dar Es Salaam,
Tel: +255222132537/2110120/211T
Email: Coi@tira.go.tz

**Zanzibar Office**
TIRA House, Kilimani
Street,P.O. Box 133 Zanzibar,
Tel: +255 24 2237271,
Fax: +255 242237272,
Email: dcoi@tira.go.tz

**Lake Zone**
5thFloor, PPF House, Kenyatta Road
P.O.Box 114, Mwanza,
Tel: +255282506000
Email: lake@tira.go.tz

**Northern Zone**
NSSF Building Kaloleni, 5th Floor,
P. O. Box 15468, Arusha,
Tel: +255272520017,
Email: northern@tira.go.tz

**Southern Highlands Zone**
NHIF Building, Karume Avenue,
4th Floor, P.O.Box 1618 Mbeya,
Tel: +255 252957324
Email: southern@tira.go.tz